The University of Osaka
Institutional Knowledge Archive

| Title | Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili |
|---|---|
| Author(s) | Isack, Zainabu Kassu |
| Citation | 外国語教育のフロンティア. 2018, 1, p. 105-118 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/69783 |
| rights | |
| Note | |

*The University of Osaka Institutional Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

The University of Osaka

# Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili
## (The Upbringing and Life Stages in Swahili Culture)

ISACK, Zainabu Kassu

**Iksiri**

Utamaduni ni jumla ya mila, desturi na mitindo ya maisha ya watu wa jamii fulani. Utamaduni unaangalia namna watu wanavyofanya mambo yao kwa kawaida kama vile; wakati gani au nini wanakula, mavazi yao, wanasalimiana vipi, mambo ambayo ni adabu, miiko yao, mambo wanayoamini n.k. Mambo ambayo yanaweza kuutambulisha utamaduni wa watu wa jamii fulani ni mengi na anwai, kujaribu kuyazungumzia yote kwa kina na mapana yake katika makala fupi kama hii ingekuwa ni kazi isiyo na tija. Dhati ya makala hii basi, ni kuangazia kipengele kimoja tu cha utamaduni wa Kiswahili; *Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili*. Ufafanuzi wa kipengele hicho unakusudiwa kuwanufaisha wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Msukumo wa kazi hii umetokana na changamoto za mwandishi katika uzoefu wake wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na utamaduni wake kwa wanafunzi wageni. Changamoto hizo hasa ni kutokana na uhaba wa zana za kufundishia, hususan rejea zinazohusu maarifa juu ya utamaduni wa Kiswahili, zinazowalenga wajifunzaji na wafundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Ni dhahiri kuwa tunapojifunza lugha ya kigeni tunajifunza utamaduni wake pia, hivyo umuhimu wa kuwa na rejea za maarifa ya utamaduni wa jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili ni jambo linalohitaji kupewa uzito katika maandishi ya Kiswahili. Kazi hii ichukuliwe kama chachu tu ya kuhamasisha uandishi wa kina na endelevu juu vipengele vingine vinavyotuangazia maarifa juu ya utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla.

**Abstract**

Culture is the sum total of social behaviors, traditions, customs and a total way of life of a particular society. It looks at the regular practices of the given society such as; when or what they eat, their dress codes, greetings, their etiquettes, taboos, their beliefs and so on. Aspects that can help us in identifying a culture of a certain society are many and diversified and thus it would be a futile task trying to cover them in depth in a brief article like this. It is in that light thus, this article highlights only one aspect of Swahili Culture: *Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili* (The Upbringing and Life Stages in Swahili Culture). Both instructors and learners of Swahili as a foreign language are expected to benefit from the description of such an element of culture. The writer was driven to write on the subject by the challenges she has been facing through

teaching Swahili and Swahili Culture to the foreign students. The challenges specifically were due to the lack of enough reference materials on Swahili Culture aimed for learners and instructors of Swahili as a Foreign Language. The fact that when we learn a foreign language we also learn its culture is obvious, thus having references on the culture of the native speakers of Swahili is prime in Swahili literature. This work should be taken as a catalyst for an in depth and sustainable literature on other aspects of Swahili Culture and African Culture at large.

Keywords: Utamaduni wa Kiswahili, Makuzi, Hatua za Maisha

**1. Utangulizi**

Kwa sababu ya uchangamano wa mfumo wake, nafasi, dhima na uamilifu wake kwa jamii, lugha imetokea kuwa jambo lililowavutia sana binadamu, tangu zama za kale sana, kuitafiti, kuichambua na kuifafanua ili kujua asili, undani na mabadiliko ya mfumo wake, pamoja na nafasi na dhima zake (Mekacha 2000:5). Lugha ya Kiswahili pia haighairi ukweli huu. Kiswahili kama moja ya lugha kubwa za Kiafrika ni lugha ambayo imekuwa ikiwavutia watu wengi. Hatuwezi kupingana na ukweli kuwa lugha hii na ufundishaji wake ina dhima muhimu na nafasi nzuri hasa katika zama hizi kutokana na utandawazi: yaani azma ya kuinganisha dunia kama kijiji kimoja. Lugha hii imeenea na imefanikiwa kwa kiasi fulani si tu ndani ya Afrika ya Mashariki ambamo ndimo ilimochipukia, bali pia imevuka mipaka ya Kitaifa na Kimataifa. Kama asemavyo Mtesigwa (2005:74) akielezea matumizi ya Kiswahili katika nchi za maziwa makuu, ninamnukuu: "Kiswahili kimekuwa kikiendelea kutumika kwa mawasiliano baina ya wenyeji wa nchi hizi na kutokana na na kuenea kwake na kuvunja mipaka ya kikabila na kitaifa, ni lugha yenye sifa ya kuweza kukuza umoja katika nchi hizi". Jambo hilo linaungwa mkono na Kihore (2005:388) ninamnukuu: "Kiswahili kimekwishafikia hatua ambazo hakiwezi kurudishwa nyuma hivihivi. Hii ina maana kuwa lugha hii imekwisha ingia katika utandawazi wa kuwaunganisha wananchi wa nchi za Afrika ya Mashariki, Kati na Kusini". Kihore (kashatajwa) anaendelea kuongeza kuwa: "Kiswahili pia kimeingizwa katika utandawazi kutokea juu na vyombo kama vile Vyuo Vikuu vya nchi za ng'ambo na vyombo vingine mbalimbali kama intaneti na radio za nchi kubwa".

Kutokana na unyeti wa dhima yake na nafasi ya Lugha ya Kiswahili katika ulimwengu wa sasa, ni dhahiri kuwa Kiswahili na ufundishaji wa Kiswahili unapaswa kuimarishwa. Njia mojawapo na ambayo ndiyo msingi wa makala hii, ni haja ya kuwa na maandishi ya Kiswahili kuhusu mada na maarifa mbalimbali yanayokidhi soko lake, na mahitaji ya wajifunzaji wa Kiswahili na Utamaduni wake. Makala hii inakusudia kuangazia kipengele kimojawapo cha Utamaduni wa Kiswahili: *Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili*. Ufafanuzi wa kipengele

hicho unakusudiwa kuwanufaisha wakufunzi na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama Lugha ya Kigeni. Msukumo wa uteuzi wa mada hiyo umetokana na changamoto za mwandishi katika uzoefu wake wa takriban miaka 10, katika ufundishaji wa Kiswahili na Utamaduni wake kwa wanafunzi wageni. Changamoto hizo hasa ni kutokana na uhaba wa zana za kufundishia, hususan rejea zenye maudhui kuhusu Utamaduni wa Kiswahili zinazowalenga wajifunzaji na wafundishaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni.

## 2. Usuli

Sehemu hii inaelezea kwa ufupi mambo matatu: Kwanza, ni yepi malengo ya wajifunzaji wa lugha ya Kigeni. Pili, kufasili maana ya utamaduni na kufafanua kwa nini ni muhimu kujifunza utamaduni wa jamii fulani hasa kwa mwanafunzi wa lugha, na mwisho tutataja baadhi ya mambo ya msingi yanayoutambulisha utamaduni wa watu.

Kwa kawaida ujifunzaji na ufundishaji wa Lugha ya Kigeni una malengo mbalimbali miongoni mwa wanafunzi na hata walimu. Kati ya malengo hayo ni: kutaka kuwasiliana na wenyeji wa lugha ile, kujiandaa kusafiri ng'ambo kwa ziara za utalii, biashara au shughuli maalumu za kikazi, kutaka kusoma na kufahamu fasihi iliyo katika lugha hiyo, kujua lugha hiyo na kuitumia kama lugha ya kujifunzia masomo au maarifa maalumu yanayotolewa katika lugha hiyo, kutimiza masharti ya kufuzu mafunzo ya kiwango fulani kama vile shahada, hasa katika idara zinazofundisha lugha katika vyuo n.k (Mtesigwa 2009) Malengo mengine yanaweza kuwa; kuweza kufanya utafiti katika taaluma ya lugha husika na kuweza kupata ajira inayomhitajia mtu kutumia lugha hiyo.

Tunapoanza kujifunza lugha yeyote kwa kawaida tunalenga stadi kuu nne katika mfuatano, yaani: kwanza stadi ya kusikiliza, halafu kusoma, kisha kusema na hatimaye kuandika. Hata hivyo, katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni tunasisitiza ni muhimu kuongeza stadi moja zaidi, nayo ni stadi ya Utamaduni. Utamaduni ni nini? Tunaweza kusema utamaduni ni jumla ya tabia, mila, desturi na mitindo ya maisha ya watu wa jamii fulani kwa ujumla. Utamaduni unaangalia namna watu wanavyofanya mambo yao kwa kawaida kama vile; wakati gani au nini wanakula, mavazi yao, wanasalimiana vipi, mambo ya adabu na miiko, mambo wanayoamini na kadhalika.

Lengo la msingi lisilobadilika kwa yeyote anayeamua kujifunza Lugha ya Kigeni ni kupata umilisi wa kuitumia ili awasiliane na wenyeji wa lugha hiyo kwa mahitaji haya au yale. Na ili aweze kufanya hivyo, inambidi awe na umilisi wa kiisimu ili aiseme lugha hiyo kwa usahihi. Lakini umilisi wa kiisimu peke yake hautoshi kumwezesha kuwasiliana na wazungumzaji wenyeji wa lugha ile kikamilifu kwa kuwa lugha si kujua kanuni zake za kiisimu tu. Mwanafunzi wa Lugha ya Kigeni anapaswa pia kuwa na umilisi wa kimawasiliano. Aina hii ya umilisi inahitaji kuhusisha mambo mengi hasa kuhusu utamaduni wa wenyeji wa lugha ile zaidi ya kujua kanuni

za sarufi (Mtesigwa 2009). Kwa mantiki hiyo, ikiwa mtu ana malengo ya kujifunza lugha fulani ya kigeni kama ilivyodokezwa hapo juu, ni muhimu sana kuwa na utajirisho wa utamaduni wa jamii husika. Tunaweza kusema lugha ni kipengele kimojawapo cha utamaduni wa jamii fulani. Na kama tujuavyo hatuwezi kutenganisha lugha na jamii, kwani ni vitu viwili vyenye uhusiano wa karibu. Ni mambo gani yanatutambulisha utamaduni wa watu? Kimsingi, kuna vipengele vingi sana vinavyoweza kuutambulisha utamaduni wa watu. Katika makala hii tutataja baadhi yake tu, mambo hayo ni kama vile; desturi za maamkizi, chakula, mila za makuzi, desturi katika hatua mbali mbali za maisha, mambo yahusuyo dini, imani na falsafa ya maisha, fasihi, sanaa nyingine na burudani za jamii husika, mambo ya adabu na miiko na kadhalika.

Katika sehemu ifuatayo tumeteua kuangazia kipengele kimojawapo tu cha utamaduni wa Kiswahili, nacho ni *Makuzi na Hatua za Maisha*. Ni muhimu kueleza kuwa dhana ya utamaduni wa Kiswahili katika makala hii inajumuisha mila, desturi, na jadi zilizoenea na zenye uwiano katika sehemu mbali za Uswahilini aghalabu katika miji ya upwa wa pwani ya Afrika Mashariki na hasa mila na desturi hizo zikifungamana kwa kiasi kikubwa ya dini ya Kiislamu. Hata hivyo si lengo la makala hii kuzamia katika utamaduni wa kabila fulani mahsusi, na pia mengi ya yanayozungumziwa ni kutokana na tajriba binafsi ya mwandishi; kwa kuyaona, kusikia, kuyapitia katika maisha yake, kusoma katika kazi mbali za kifasihi zinazosawiri maisha ya jamii husika na maandiko yanayohusu hadithi za kweli za maisha ya waswahili. Pale inapojuzu, nukuu za waandishi wengine zenye kuwiana na mada au kipengele fulani zimetumika.

## 3. Makuzi na Hatua za Maisha

Sehemu hii inatalii makuzi na hatua za maisha katika utamaduni wa Kiswahili kutoka kuzaliwa mpaka kufa. Kwa Waswahili maisha yana hatua nne (4) muhimu; Kuzaliwa, kukua, ndoa, na kifo. Makala inaangazia kila hatua na kujaribu kufafanua mambo muhimu ya kitamaduni yanayohusiana na kila hatua katika utamaduni wa Kiswahili. Mengi ya mambo hayo yanafungamana kwa kiasi kikubwa na athari ya dini ya Kiislamu na mila na desturi za kijadi ambazo hazihusiani na dini ya Kiislamu. Mila na desturi zinazofungamana na dini nyingine zipo nje ya mawanda ya mjadala wa makala hii.

### 3.1 Kuzaliwa

Hii ni hatua ya mwanzo kabisa katika maisha ya mwanadamu. Maisha yanaanza pale mtoto anapozaliwa. Kwa Waswahili hili ni tukio la furaha sana. Pindi mtoto anapozaliwa, huadhiniwa katika sikio la kulia na hukimiwa katika sikio la kushoto (adhana na ikama ni wito wa kwenda katika ibada ya swala kwa waislamu). Pia kuna desturi ya kuwalambisha watoto asali na shubiri

wanapozaliwa desturi hii inasemekana ni moja ya "sunna" yaani matendo aliyofanya mtume Muhammad (rehma na amani iwe juu yake) kwa watoto wanapozaliwa. Na watoto hunyolewa nywele na kufanyiwa *hakika* yaani kafara ya mnyama kama mbuzi au kondoo. Watoto hupewa jina ndani ya siku 7 kwa kawaida. Utoaji wa jina ni jambo muhimu, watu huwapa watoto majina ya maneno yenye maana fulani katika lugha ya Kiswahili, majina ya watu muhimu katika historia ya uislamu au kwa kuwarithisha jina la mtu katika ukoo kama vile bibi, babu, shangazi n.k. Kwa jumla majina ya Kiswahili yana maana fulani. Ifuatayo ni mifano ya majina hayo na maana zake;

**Jedwali la 1 Mifano ya majina ya Kiswahili na Maana zake**

| Na. | Jina | Asili | Maana |
|---|---|---|---|
| i. | Zawadi | Kiswahili | Mtoto wa kike huyo ni sawa na zawadi kutoka kwa Mungu |
| ii | Asumini | Kiswahili | Jina la kike, lina maana ya ua la muasumini |
| iii. | Chausiku | Kiswahili | Mtoto wa kike aliyezaliwa usiku |
| iv. | Mwanamvua | Kiswahili | Mtoto wa kike aliyezaliwa wakati wa mvua |
| v. | Mwanaidi | Kiswahili | Mtoto wa kike aliyezaliwa wakati wa sikukuu ya kiislamu, Iddi |
| vi. | Fatuma | Kiislamu | Jina la kike la Kiislamu, jina la mtoto wa mtume Muhamad |
| vii. | Hadija | Kiislamu | Jina la kike la Kiislamu, jina la mke wa mtume Muhhamad |
| viii. | Musa | Kiislam | Jina la kiume la Kiislamu, jina la mmoja wa mitume |
| ix. | Mwapili | Kiswahili | Mtoto wa kike wa pili kuzaliwa |
| x. | Hidaya | Kiswahili | Mtoto wa kike, lina maana ya uongofu, tunu, hiba, zawadi. |

Mwanamke aliyetoka kujifungua huitwa *mzazi*, aghalabu kwa siku arobaini za mwanzo na mpaka miezi mitatu ya mwanzo. Chakula cha mzazi kwa desturi ni chakula cha moto na laini kama; supu, uji na chai yenye pili pili manga. Mzazi anahitajiwa kula chakula vizuri ili kurejesha damu aliyopoteza na kupata nguvu. Waswahili wanaamini ikiwa mzazi atakula chakula cha baridi, basi jambo hilo litaathiri utengenezaji wa maziwa kwa ajili ya kumnyonyesha mtoto. Kidesturi mtoto hunyonya maziwa ya mamaye na ukomo wake ni mtoto anapofika miaka miwili.

Pia, ni desturi kwa mzazi kukoga maji moto baada ya kujifungua na kuendelea kukandwa kwa maji moto na kupakwa mafuta aghalabu kwa siku saba za mwanzo. Shughuli hii hufanywa na mkunga, mama wa mzazi au jamaa wa karibu anayemsaidia mzazi. Zamani pia watu hawakuwa na desturi za kuzalia hospitalini. Mkunga angeitwa nyumbani na kumzalisha pamoja na kumkanda mzazi kwa ujira kidogo. Desturi nyingine, ni kufunga tumbo *mkaja* baada ya kujifungua. Waswahili wanafikra kuwa kufunga huko kutalirejesha tumbo katika hali yake ya awali kabla ya ujauzito.

Kwa kawaida mzazi na mtoto aliyezaliwa hukaa ndani bila kwenda nje ya nyumbani (isipokuwa kwa dharura) kwa siku arobaini. Katika imani ya kiislamu ndani ya siku hizo, mzazi ana sharti la kuoga pindi anapomaliza damu ya uzazi ili kujitoharisha (kujiweka safi). Hawezi kuswali au kusoma kurani kutoka anapojifungua mpaka anapooga josho la nifasi (yaani kuoga ili kujiweka

tohara baada ya kujifungua). Siku ya arobaini ni sherehe ya kumtoa mtoto ambayo hujulikana kama *arobaini ya mtoto*. Wakati wa arobaini ndugu, jamaa, na marafiki huja pamoja na kumfanyia mtoto maulidi au kisomo. Mama na mtoto hupewa zawadi kama pesa au khanga. Arobaini ni sherehe ya kufurahia ujio wa mtoto, na kumpongeza mama pia.

### 3.2 Kukua

Hii ni hatua muhimu pia katika maisha ya waswahili. Kidini watoto wanahitaji kupewa elimu ya dunia yaani shuleni na elimu ya akhera yaani elimu ya dini itolewayo katika vyuo vya dini (madrasa). Elimu ya dunia yaani shule ni ya kumwandaa mtoto kuishi vyema hapa duniani, aghalabu kwa kupata kazi na kipato cha kuendesha maisha yake. Na elimu ya dini ni ile inayomfunza kuzingatia misingi ya dini katika maisha yake ya kila siku hapa duniani na maandalizi ya maisha yake kesho akhera. Watoto huanza kufundishwa mapema aghalabu kuanzia miaka mitano hivi, lakini huwa na wajibu na majukumu kamili kama watu wazima pale wanapofikia hatua ya kukua. Mtoto husemekana amekua pindi anapofikia umri wa *kubalehe* au *kuvunja ungo* kwa mtoto wa kike. Yaani anapopevuka kimwili.

Kwa upande mwingine, kitamaduni watoto hupewa mafunzo kupitia jando na unyago. Lakini jando na unyago ni nini? *Jando* na *unyago* ni mila ya mafunzo ya siri wapewayo vijana walio katika rika la balehe, mafunzo hayo yanalenga kumwandaa kijana kukabiliana na maisha ya utu uzima. Mila ya unyago hususan imeenea si tu Uswahili, lakini hata katika baadhi ya makabila ya kibantu kama katika jamii ya Wamakonde (kabila linalopatika Kusini-Mashariki mwa Tanzania na Kaskazini mwa Malawi). Kwa mfano, katika *Mwendo* (Lema 1998:42) shangazi wa Felisia (mmoja wa wahusika) anamwelezea Felisia kuhusu unyago kwa kusema, “Unyago ni jadi. Unyago ni daraja. Linakutoa katika dunia ya utoto, linakuvusha na kukufikisha katika dunia ya utu uzima. Usipovuka hilo daraja unabaki umetekwa nyara katika dunia ya watoto”.

Jando, ni mafunzo kwa vijana wa kiume, ni mafunzo ya siri; vijana wa kiume na wanaume pekee ndio waruhusiwao kuingia katika mafunzo hayo. Mtu anayewapa mafunzo hayo huitwa *kungwi* au *ngariba*. Mafunzo haya humwandaa kijana kuwa mwanamume, mume, baba bora. Pia, humfunza stadi au sifa anazohitaji kama mwanamume kadiri ya miwani ya uanaume katika macho ya jamii. Sifa hizo ni pamoja na kubeba jukumu kama kiongozi katika familia, ujasiri, kujiamini katika kufanya maamuzi, mambo yahusuyo ndoa, na maisha kwa ujumla. Mafunzo ya jando huambatana na *tohara*. Ijapokuwa jando ni mila au jadi maalum ya makabila mbalimbali ya Kiafrika, tohara kwa upande mwingine ni mila muhimu kwa wanaume wa Kiswahili hata sasa. Mila hii ina taathira ya dini ya Kiislamu, ni katika ada za wanaume wa Kiislamu. Kijamii, ni aibu na fedheha kwa mwanamume kutokufanyiwa tohara. Tohara inatazamwa kama sehemu ya ukamilifu

wa kuwa mwanaume bora.

Unyago kwa upande mwingine ni mafunzo ya siri kwa watoto wa kike. Msichana ambaye ni rika la kuingia katika mafunzo ya unyago huitwa *mwari*, na mtu anayemfunda mwari huitwa *kungwi* au *somo* wake. Mafunzo ya unyago humuandaa binti kuwa mwanamke, mama, na mke bora katika viwango vya jamii husika. Mambo anayofundishwa msichana ni pamoja na; usafi wake binafsi, usafi wa nyumba, mapishi, ulezi wa watoto, kumtunza mume, namna ya kuishi na watu wengine, adabu, mambo ya ndoa na maisha kwa jumla. Aghalabu mafunzo haya hufanyika kwa njia ya ngoma na vitendo na huweza kuchukua kati ya siku kadhaa mpaka miezi. Mafunzo haya pia ni sherehe maarufu kama *ngoma* (ya unyago) au *kuchezwa*. Unyago pia ni pongezi kwa wazazi kwa kumkuza binti. Zamani ilitarajiwa kuwa msichana atapata mume mara baada ya kuwa mwari.

Mila na desturi za jando na unyago zinafifia katika zama hizi kutokana na ukweli kuwa watoto wa rika la kufundwa unyagoni wapo shuleni. Hata hivyo, mambo ambayo wasichana na wavulana wanapaswa kufunzwa pamoja na desturi ya tohara bado zinashikiliwa na kutolewa kwa njia mbali mbali nje ya sherehe kamili za jando na unyago. Njia hizo ni pamoja na mafunzo nyumbani kutoka kwa wazazi au ndugu wengine kama bibi au shangazi. Kumpeleka binti kwa kungwi akafundwe aghalabu wakati wa likizo mara baada ya kubalehe, kumfunda mwari au bi harusi mtarajiwa kabla ya harusi, kumfanyia mtoto wa kiume tohara hospitalini katika umri mdogo kabla ya balehe na kadhalika.

### 3.3 Ndoa

Ndoa ni ada nyeti na hatua muhimu katika maisha ya Waswahili. Kiislamu ndoa inaelezwa kama ni nusu ya dini. Kuoa kunachukuliwa kama ndio namna ya kupata utulivu wa nafsi na kupata stara. Kitamaduni, ndoa ni tukio la furaha na heshima kwa wazazi. Kama anavyoandika Sengo (1992:53) akifafanua maoni ya Mbaabu (1985) kuhusu ndoa na harusi katika utamaduni wa Kiswahili ninamnukuu, "Ndoa na Harusi: Uswahilini ni taasisi ya kwanza kwa uzito wa maisha ya kila siku ya mtu. Ubikira ni ada kubwa sana kwa wasichana wa Kiswahili kabla ya kuolewa kwani ndoa ndicho kitovu cha maisha ya Waswahili. Ni desturi iliyoenea mwote Uswahilini, kwa wazazi kuwa washauri wakuu wa ndoa za watoto wao". Kama asemavyo Mbaabu (kashatajwa), wazazi ndio washauri wakuu katika masuala ya ndoa. Zamani wazazi waliweza hata kumchagulia kijana wao, au binti yao mwenza na watoto walitarajiwa kukubali bila kuwapinga. Aghalabu familia zenye urafiki baina ya wazazi zingewaozesha watoto wao ili kudumisha urafiki wao. Ndoa huchukuliwa kama ndio namna pekee inayoheshimika katika kuendeleza kizazi. Kidini na kitamaduni si maadili kujihusisha na mapenzi kabla ya ndoa, nje ya ndoa na pia kupata mtoto kabla ya ndoa au nje ya ndoa. Dini ya Kiislamu ina nafasi kubwa katika maisha ya ndoa. Kwa mfano, Mbaabu (1985)

akirejelewa katika Sengo (1992:53) anafafanua kwamba, “Kwa waumini wa kweli wa Uislamu sharia za Kiislamu huwa ndicho kigezo pekee cha kuendesha maisha ya ndoa”. Kidesturi watu wanatumaini kuwa mtapata watoto katika ndoa. Ndoa yenye kuleta watoto huitwa ndoa yenye matunda (mafanikio) na aghalabu ndoa isiyo na watoto ni chanzo cha mifarakano mikubwa katika familia, na hasa imekuwa desturi kwa mke kuangushiwa mzigo wa lawama katika kadhia kama hizo.

### 3.3.1 Utaratibu wa ndoa

Ndoa za Kiswahili au za Kiafrika kwa ujumla zina utaratibu au hatua kadhaa maalum za kufuata tangu mtu anapotoa posa mpaka anapofunga ndoa au kufanya harusi. Katika Sehemu hii tutazungumzia kwa kifupi kila hatua au jambo muhimu katika mila na desturi za ndoa za Kiswahili au Kiafrika kwa jumla pale inapojuzu kujumuisha.

#### 3.3.1.1 Posa na Uchumba

Kwanza ni hatua ya kuposa. Kijana wa kiume anapofikia umri wa kuoa au anapopata msichana anayempenda na akataka kumwoa, hawezi kwenda moja kwa moja kwa wazazi wa msichana huyo. Anahitaji kutoa *posa* kwanza. Posa ni maombi au ruhusa ya kutaka kuoa, maombi hayo hupelekwa kwa wazazi wa msichana. Basi, kijana wa kiume humtafuta *mshenga*; yaani mwanaume, mtu mzima, anayeheshimika katika jamii, na aghalabu mlumbi wa maneno. Mshenga hupewa barua ya posa na kuipeleka kwa wazazi wa msichana. Ikiwa mazungumzo baina ya mshenga na wazazi yatakwenda vizuri, basi wazazi husemekana wamekubali posa. Na hapo, wazazi huwatajia familia ya kijana wa kiume, *mahari* inayohitajika. Mahari ni zawadi inayotolewa na kijana wa kiume kwenda kwa msichana au familia ya msichana anayetarajia kuolewa. Mahari aghalabu huwa kitu cha thamani kama vile; pesa, vito vya thamani, mifugo n.k. Kiislamu mahari ni zawadi ya msichana anayeolewa, naye ana uchaguzi wa kuamua mahari anayoitaka na hupewa mahari hiyo yeye mwenyewe, hilo ni sharti moja la ndoa ya Kiislamu. Kwa upande mwingine, katika mila nyingi za Kiafrika, mahari ni zawadi na shukrani kwa wazazi na walezi wa msichana, kwa hivyo mahari hiyo huamuliwa na familia au wazazi wa upande wa msichana na huenda kwao. Ikiwa posa imekubaliwa na mambo ya mahari na siku ya ndoa imeafikiwa, kijana na msichana huhesabiwa wamefikia hatua ya *uchumba* au wao ni wachumba. Familia za kijana na msichana huweza kukutana na kutambulishana na kusherehekea hatua hii.

#### 3.3.1.2 Ndoa na Harusi

Hatua ya pili, ni ndoa yenyewe. Hapa tutazungumzia zaidi ndoa za kiislamu. Katika ndoa za

Kiislamu ili ndoa ikamilike sharti kuwe na kijana (mwanamume) anayeooa yaani bwana harusi, na msichana (mwanamke) anayeolewa yaani bibi harusi, halafu pawe na mtu anayefungisha ndoa aghalabu shekhe, pawe na mashahidi wanaume wawili, pawe na walii yaani mtu anayetoa idhini ya kumruhusu binti kuolewa aghalabu walii ni baba, au kaka, mlezi wa binti na sharti la mwisho ni kuwe na makubaliano kuhusu mahari au malipo ya mahari kwa binti anayeolewa.

Wakati wa ndoa mwanaume huulizwa mara tatu kama fulani bin fulani (yaani majina yake bwana harusi) umekubali kumwoa fulani binti fulani (yaani majina ya bibi harusi) kwa mahari mliyokubaliana? Na endapo bwana harusi atajibu Naam, katika mara zote tatu, hapo tunasema tayari ndoa imeshafungwa. Kirasmi nchini Tanzania, wana ndoa hupewa cheti cha ndoa na taasisi ya dini, na huhitaji pia kuandikisha ndoa hiyo serikalini na kupewa cheti cha serikali na mamlaka inayohusika na usajili wa ndoa pia. Kijamii shughuli rasmi ya ndoa huenda pamoja na sherehe ya harusi. Katika harusi, baada ya ndoa kufungwa watu hula chakula aghalabu kilichoandaliwa na familia ya bibi harusi, kwani kwa kawaida ndoa za Kiislamu hufanyika kwa bibi harusi.

Kitamaduni, ndoa na harusi ni tukio kubwa la furaha, na tukio muhimu la kijamii. Katika harusi za kiafrika kwa ujumla ndugu, jamaa, marafiki na hata majirani hujumuika pamoja. Na ni muhimu sana kwa watu kushirikiana katika matukio kama haya. Kutokwenda katika harusi za ndugu, jamaa, hata jirani zako, si vizuri huchukuliwa kama ishara ya uhusiano mbaya machoni mwa jamii za waswahili na waafrika kwa ujumla.

Kitamaduni, harusi huweza kuendelea kwa siku 3 hata 7. Harusi husherehekewa kwa kula, kunywa, kuwapa zawadi wazazi na maharusi (yaani bwana na bibi harusi) na burudani mbali mbali. Watu huimba na kucheza nyimbo za furaha kama vile za kuwapongeza wazazi na maharusi, na kuwaombea maharusi kuwa na maisha mazuri na kizazi chema.

Maharusi hupumzika na kukaa ndani kwa siku saba baada ya ndoa. Kipindi hiki huitwa *fungate.* Pia, mara baada ya ndoa kufungwa katika ada za Waswahili, ndio wakati wa kutambua ikiwa ndoa imehongera au la! Yaani ikiwa msichana atakutwa akiwa bikra (hakuwahi kuingiliwa kimwili na mwanamume) na kwake ni mara ya kwanza kukutana kimwili na mumewe, basi Waswahili husema ndoa imehongera! Mila hii, inasawiriwa barabara katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (Mohamed 2000). Bi. Haja aliye mmoja wa wahusika anapika vitumbua na kuvitia mchanga kwa makusudi, ili kufikisha ujumbe wake kisitiari. Msichana ambaye si bikra anatazamwa kama mwenye dosari machoni mwa jamii na anafananishwa na kitumbua kilichoingia mchanga: hakiliki. Ubikira ni jambo lililoshikiliwa sana zamani kama alama ya heshima kwa waliomlea na usafi kwa msichana. Hata hivyo, mila hii imefifia katika siku za karibuni.

Katika ndoa za Kiislamu na baadhi ya jamii za kiafrika kuna utamaduni wa ndoa za *mitara*.

Ndoa za mitara ni ndoa zinazoruhusu mwanamume kuoa mke zaidi ya mmoja. Kwa upande wa Kiislamu, mwanamume anaruhusiwa kuoa hadi wanawake wanne, kwa sharti la kuwa mwadilifu na kutenda kila jambo kwa usawa baina ya wake zake, na ikiwa hawezi basi anashauriwa abaki na mke mmoja. Wanawake walioolewa na mume mmoja huitwa *wake wenza*. Mke wa kwanza akiitwa mke mkubwa na wanaofuatia wake wadogo au kwa kuzingatia nafasi yake: mke wa pili, mke wa tatu na mke wa nne (mke wa mwisho).

**3.3.1.3 Talaka**

Watu wanatarajia baada ya ndoa mke na mume wataishi maisha yao yote kwa amani na furaha na watapata watoto. Hata hivyo endapo mke na mume watakuwa na magomvi yasiyoweza kusuluhishwa, katika ndoa za Kiislamu, mume anaweza kutoa *talaka*. Talaka ni hati au tamko la mume mbele ya mashahidi la kuonyesha kutaka kumwacha mke ama kwa talaka moja, mbili au tatu. Mwanamume anapotoa talaka mara ya kwanza (talaka moja) au ya pili talaka hiyo huitwa *talaka rejea*. Mwanamke anapaswa kukaa tohara 3 baada ya kupewa talaka. Kipindi hiki huitwa *eda* ya kuachwa. Hekima ya kukaa miezi mitatu ni kuhakikisha mke huyo si mjamzito, pia kuwapa mume na mke muda wa kutafakari pengine wakasameheana na kurejeana. Mume sharti amtunze mke katika kipindi chote cha eda kwani bado huhesabiwa ni mkewe. Katika kipindi cha eda ya talaka rejea pia, mke na mume huweza kukaa katika nyumba moja na kuendelea na maisha ya kila siku ikitarajiwa huenda wakasameheana na kuamua kuendelea na ndoa kabla ya eda kumalizika. Ikiwa hakuna suluhu baada ya talaka mbili na eda kumalizika mume humpa mke talaka ya tatu. Baada ya mume kumpa mkewe talaka 3, basi husemekana mke huyo ni haramu kwake, na hawezi kuwa mke wake tena, labda mpaka mke huyo aolewe tena na kuachika kwa talaka 3 kwa mume mwingine, ndipo mume huyu huweza kumuoa upya.

Kwa hivyo suala la talaka kwa imani ya kiislamu ni jambo linaloruhusiwa ila halikufanywa rahisi bila shaka, vile vile ni jambo lisilopendwa kidini na hata kijamii. Baada ya kumwacha mke katika imani ya kiislamu, si sawa kuchukua mali au zawadi mume alizompa mkewe. Na wana ndoa wanashauriwa kuishi kwa wema na ikitokea wameshindwa basi waachane kwa wema.

Mamlaka ya kutoa talaka kiislamu na kitamaduni katika jamii nyingi za Kiafrika ni ya mwanamume. Hata hivyo ikiwa mke hataki kuendelea kuwa katika ndoa kwa sababu moja au nyingine katika imani ya kiislamu, mke huyo anaweza kujivua katika ndoa, kitendo hicho hujulikana kama *khulu'u* katika sharia za kiislamu. Ili kujitoa katika ndoa mke anapaswa kurejesha mahari aliyopewa wakati wa ndoa kama sharti la kujivua huko. Hata hivyo, katika nchi kama Tanzania hata kwa Waislamu, mahakama ndiyo yenye mamlaka rasmi na ya mwisho ya kuthibitisha na kutoa hati ya talaka baada ya kuendesha kesi mahakamani kwa kupokea mashauri kutoka

mabaraza ya usuluhishi ya taasisi za dini na ushahidi kutoka kwa wanandoa na watu wengine wenye kufahamu kuhusu ndoa husika.

### 3.4 Kifo

Waswahili huamini kifo ni faradhi (lazima) kwa kila mwanadamu. Na inafikiriwa kuwa kifo ni kichungu, katika dini ya kiislamu jambo hili husemwa kama: kila nafsi itaonja mauti. Kinyume na harusi, kifo na shughuli zinazoambatana nazo yaani *msiba* ni tukio la huzuni. Lakini kama ilivyo kwa harusi, msiba pia ni tukio la kijamii, inatarajiwa kuwa ndugu, jamaa, marafiki na hata majirani kushirikiana na kusaidia katika misiba. Ushirikiano huchukuliwa kama ishara ya uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii.

Kutokana na imani ya kiislamu, waswahili wanaamini kuwa duniani tumeletwa na Mungu, na hata mtu anapokufa basi ahadi yake imefika, (mwisho wa maisha yake ya duniani umewadia) maradhi, ajali, au uzee huchukuliwa kama sababu tu katika mtazamo wa kidunia zinazosababisha kifo. Pia huamini kuna maisha baada ya kifo, kwa maana sote marejeo yetu ni kwa Mwenyezi Mungu (akhera). Watu wanapofikwa na msiba husema misemo kama "hiyo ni kazi ya Mungu", au "sote ni wake (Mwenyezi Mungu) na kwake tutarejea" (ina lillah waina ilayhi rajiuun).

#### 3.4.1 Utaratibu wa mazishi

Kifo na shughuli zote zinazoambatana nazo hutawaliwa sana na kuongozwa na dini. Katika imani ya Kiislamu upo utaratibu maalumu katika mazishi. Katika sehemu hii tutaelezea ada muhimu zinazohusu mazishi kwa kifupi bila kueleza kila ada kiundani sana.

Mtu anapokufa yaani anapokuwa *maiti*, kwanza ni ada kuogeshwa pia hujulikana kama kuosha maiti. Aghalabu maiti mwanamume huoshwa na wanaume (ndugu, jamaa, waislamu-wanaume) na maiti mwanamke huoshwa na wanawake (ndugu, jamaa, waislamu-wanawake). Kisha maiti huvishwa sanda, yaani kumsitiri maiti aghalabu kwa shuka nyeupe, na inasemekana kama ni vizuri kumfukiza au kumtia manukato pia. Tatu, ni swala ya maiti, mwislamu yeyote anapokufa ni ada kuswaliwa kabla ya kuzikwa kaburini. Mwisho, ni kuzika: jinsi ya kuzika kwa uchache ni kumzika maiti katika shimo linalozuia harufu na kumlinda na wanyama kutomfukua. Kutolewa maiti katika jeneza kabla ya kuzikwa ni kaida, yaani waislamu hawazikwi na jeneza. Na desturi ya kujengea kaburi juu, na kutia chokaa si katika ada za kiislamu. Hata hivyo, ni wajibu kumuelekeza maiti *kibla* (uelekeo wa Kaaba, Makka upande wanaoelekea Waislamu wakati wa swala) wakati wa kumzika. Zaidi, shughuli za mazishi hufanywa na wanaume, wanawake hawapaswi kwenda makaburini wakati wa mazishi.

### 3.4.2 Mila na desturi nyingine kuhusiana na Msiba

Katika sehemu hii tutagusia mila na desturi nyingine zinazohusiana na misiba. Baadhi ya mila na desturi hizo zina taathira ya dini hata hivyo mila na desturi nyingine ni za kijadi na hazifungamani moja kwa moja na dini. Kwanza, ni kuhusiana na mavazi: Mavazi ya msibani kitamaduni ni mavazi ya heshima, yaani mavazi yanayofunika sehemu kubwa ya mwili aghalabu hii ni taathira ya dini ya kiislamu. Wanawake kwa kawaida huvaa mavazi kama buibui, khanga mbili na kilemba au mitandio ifunikayo vichwa na sehemu ya kifua. Hata kwa wanawake wasio waislamu huheshimu desturi hii wanapokwenda katika misiba. Wanaume huvaa kanzu, suruali na shati au fulana. Pili, rangi za msiba ni rangi nyeusi ambayo huashiria huzuni au rangi nyeupe ambayo huchukuliwa kama ishara ya usafi. Tatu, Waswahili wana mila ya kulala nyumbani kwa mtu aliyefikwa na msiba kwa siku tatu, jambo hili ni ishara ya maombolezo. Mila hii hujulikana kama kulala *matanga*. Siku ya nne hujulikana kama siku ya *kuanua matanga* yaani mwisho wa kulala matanga. Nne, kuna mila ya kumwombea dua mtu aliyekufa siku ya arobaini tangu kuzikwa kwake yaani *arobaini* ya marehemu. Tano, kuhusu majina; mtu aliyefikwa na msiba hujulikana kama *mfiwa* kwa jumla; ikiwa ni mtoto aliyefiwa na wazazi huyo huitwa *yatima*. Mwanamke aliyefiwa na mume au mwanamume aliyefiwa na mke hujulikana kama *mjane*. Sita ni kuhusu *eda* ya kufiwa. Mwanamke ambaye amefiwa na mumewe hupaswa kukaa *eda* ya miezi minne na siku kumi. Eda ya kufiwa ni mila yenye taathira ya dini ya kiislamu. Kama ilivyo kwa mwanamke aliyeachwa kwa talaka, eda ni kipindi cha kusubiri bila kuolewa. Kwa mjane, hiki ni kipindi cha kuonyesha huzuni kwa mumewe na kipindi cha kuhahakisha ikiwa mke huyo aliyefiwa si mjamzito pia ili kuepusha utata wa nasaba ya mtoto ikiwa mke ataolewa tena. Ikiwa mjane yu mjamzito eda yake inatajwa kuwa huisha pindi anapojifungua.

## 4. Hitimisho

Katika makala hii tumebainisha kuwa suala la lugha ni jambo linalowavutia binadamu tangu kale. Miongoni mwa mambo yanayowavutia watu kuhusu lugha ni nafasi na dhima ya lugha husika. Makala hii imefafanua kwa ufupi kuwa lugha ya Kiswahili ina nafasi nzuri na dhima muhimu katika ulimwengu wa sasa, hasa kutokana na azma ya utandawazi. Hivi sasa, Kiswahili kimevuka mipaka ya kitaifa. Ili kuendana na hali na mahitaji ya sasa makala inapendekeza kuwa lugha ya Kiswahili pamoja na ufundishaji wake havina budi kuimarishwa. Njia moja ya utekelezaji wa hilo, kwa mujibu wa mwandishi ni haja ya kuwa na maandishi kuhusu mada na maarifa mbalimbali ya lugha ya Kiswahili na Utamaduni wake. Kwa kuonyesha mfano wa juhudi hizo, makala imeangazia kipengele kimoja cha Utamaduni wa Kiswahili: *Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili*. Uteuzi wa mada hiyo umewalenga wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama

lugha ya Kigeni, kutokana na ukweli kuwa kuna uhaba wa rejea kuhusu Utamaduni wa Kiswahili zinazowalenga makundi tajwa. Mwandishi anaongozwa na mtazamo kuwa mtu anapojifunza lugha ya kigeni, kujifunza utamaduni wa lugha husika pia ni stadi muhimu kama ilivyo kwa stadi za msingi yaani; kusikiliza, kusoma, kusema na kuandika. Ni fikra ya mwandishi kuwa ni vigumu kutumia lugha ya kigeni kikamilifu hasa unapowasiliana na wazawa ikiwa hufahamu utamaduni unaofungamana na lugha hiyo.

Kwa kuhitimisha, makala hii inasisitiza kuwa katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, suala la kuwa na rejea za kutosha juu ya maarifa ya utamaduni wa Kiswahili ni jambo linalohitaji kupewa uzito katika maandiko ya Kiswahili. Kazi hii ichukuliwe kama chachu tu ya kuhamasisha utafiti na uandishi wa kina na endelevu juu ya vipengele vingine anwai vinavyotupa mwanga juu utamaduni wa Kiswahili na Utamaduni wa Kiafrika kwa jumla. Miongoni mwa mambo ya msingi ya kitamaduni yanayoweza kuangaziwa zaidi katika kazi zijazo ni pamoja na; desturi za salamu, chakula, mavazi, dini imani na falsafa ya maisha, mambo ya adabu na miiko, fasihi, sanaa nyinginezo, burudani n.k

## Marejeo


Abdulla, Muhamed Said

1975 *Mke Mmoja waume Watatu*, East Africa Publishing House, Dar es Salaam. Ally, Muhhamad (Mkusanyaji-Kijitabu), Mazishi ya Kiislam, Dar es Salaam (Hakijachapishwa).

Kihore, Yared M.K

2005 ”Utandawazi na Ufundishaji wa Kiswahili”, Katika *Nordic Journal of African Studies* 14 (3), 384-390.

Kiimbila, J.K.

1965 ”Kanuni za Kufundisha Kiswahili”, Katika *Swahili: Journal of The Institute of Swahili Research* Vol. 35 (1), 28-39, University College, Dar es Salaam.

Lema, Elieshi

1998 *Mwendo*, E&D Limited, Dar es Salaam.

Mbaabu, Ireri

1985 *Utamaduni wa Waswahili*, Kenya publishing & Book Marketing Co. Ltd, Nairobi. Mekacha, Rugatiri D.K. 2000. *Isimujamii: Nadharia na muktadha wa Kiswahili*, Osaka University of Foreign Studies, Uk.5

Mirza, Sarah & Strobel, Margareth

1991 *Wanawake watatu wa Kiswahili: Hadithi za Maisha kutoka Mombasa, Kenya*, Indiana University Press, Bloominton & Indianapolis.

Mohamed, Said Ahmed

2000 *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, Oxford University Press, Kenya.

Mtesigwa, Peter
2005 ”Utandawazi na dhima ya Kiswahili kama Lugha ya Afrika Mashariki”, Katika *Kioo cha Lugha*, Vol.3 (No. 1), 66-75.

Mtesigwa, Peter C.K.
2009 ”Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Haja ya Kuzingatia mkabala wa Mawasiliano”, Katika *Kiswahili*, Vol. 72, (No. 1).

Sengo Tigiti S.Y
1992 ”Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini Unguja”, Katika *Nordic Journal of African Studies* 1 (1), 53-79.